

TANZANIA / JUDGMENT

kn solanki transport ltd vs mohamed abdallah haidary na mwenzake 2022

tzhcld 881 29 agosti 2022

COURT
TANZLIIDECIDED
1 January 2022

Source: media.tanzlii.org · Research copy typeset by Esheria. Not court-issued or certified.

KATIKA MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA DIVISHENI YA KAZI PAR ES SALAAM MAREJEO NA. 353 YA MWAKA 2021 K.N. SO LAN KI TRANSPORT LTD..... MLETA MAO M BI DHIDI YA MOHAMED ABDALLAH HAIDARY..... MJIBU MAOMBI 1 SHABANI TULI MJIBU MAOMBI 2 HUKUMU S. M. MAGHIMBI, J. Katika shauri hili mleta maombi anaiomba Mahakama ifanye marejeo ya maamuzi yaliyotolewa na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ("Tume") katika mgogoro wa kazi Na. CMA/DSM/TEM/329/2020/161/2020 na kutolewa maamuzi tarehe 13/08/2021 na Mheshimiwa Nyang'uye, H, Muamuzi. Mbele ya Tume wajibu maombi waliwasilisha madai ya kuachishwa kazi isivyo halali wakimtuhumu mleta maombi, aliekuwa mwajiri wao kuwa aliwaachisha kazi isivyo halali. Tume baada ya kuzingatia Ushahidi uliotolewa na pande zote mbili Tume iliamua kuwa mjibu maombi aliwaachisha kazi isivyo halali wajibu maombi hivyo akaamuriwa awalipe mishahara ya miezi 12 kama fidia ya uachishwaji kazi usio halali. Baada ya kutoridhika na maamuzi ya Tume mleta maombi amewasilisha maombi haya mbele 1 ya mahakama akiomba mahakama itungeu maamuzi hayo kwa sababu kuu zifuatazo:- i, Kwamba, Mheshimiwa muamuzi alifahamu vibaya sheria na Ushahidi kuhitimisha kwamba hapakuwa na sababu ya msingi kuwaachisha kazi wafanyakazi. ii. Kwamba, Mheshimiwa muamuzi alikuwa na upendeleo katika kuchambua Ushahidi uliotolewa na mwajiri. iii. Kwamba, Mheshimiwa muamuzi alijiongoza vibaya kisheria na kihoja kuamua kwamba taratibu hazikufuatwa katika kuwaachisha kazi wafanyakazi. Shauri hili liliendeshwa kwa njia ya maandishi. Mleta maombi aliwakilishwa na Bw. Fortunatus M. Maricha, Wakili ilihali wajibu maombi waliwakilishwa na Bw. Sospeter Lufasinza, mwakilishi binafsi. Wakili Maricha aliomba kiapo cha mleta maombi kiwe sehemu ya mawasilisho yake. Katika hoja ya kwanza alieleza kuwa kielezo D2 kwa pamoja na kielezo D5 vimeainisha sababu nne zilizopelekea wafanyakazi kusitishiwa ajira zao. Alieleza kuwa mwajiri hajaridhishwa na kitendo cha Tume kijikita katika sababu moja peke yake ambayo ni kujaribu kutoka na mali ya mwajiri yaani kuvunja uaminifu. Wakili Maricha aliendelea kueleza kuwa Tume ilisahau kuwa tuhuma zozote zinaleta mashaka kwa mwajiri na hivyo mwajiri alikuwa sahihi kuwataka wafanyakazi kujibu 2 tuhuma hizo jambo ambalo walikaidi hivyo kupelekea kuachishwa kazi. Aliongezea kuwa kukaidi maagizo ya mwajiri kulitafsiriwa kuwa ni utovu wa

nidhamu na hivyo kupelekea kuachishwa kazi. Iliendelea kuelezwa kuwa waajiriwa wenyewe katika ushahidi wao wamekiri kuwa walizuiliwa getini hivyo walikuwa na jukumu la kutoa maelezo juu ya tuhuma zilizowakabili. Wakili Maricha aliongeza kuwa Ushahidi wa DW2 kwamba mjibu maombi namba moja aiikataa kupokea barua ya wito wa kujieleza (kielelezo D2) haukupewa uzito uliostahili. Katika hoja ya kwanza wakili alimalizia kwa kueleza kuwa madai kuwa wajibu maombi walikuwa polisi muda wote wakati shauri lao likiendeshwa ni ya uongo na yanalenga kupotosha ukweli. Katika hoja ya pili wakili Maricha alieleza kuwa Tume ilijielekeza vibaya kwa kuamuru mwajiri kumlipa Mjibu maombi namba mbili (Shabani Tuli) fidia ya miezi 12 ilihali alikuwa katika kipindi cha majaribio. Kwamba alipaswa kufungua mgogoro wake akijikita katika mienendo isiyoofaa katika kazi "unfair labour practice" na sio uachishwaji kazi usio halali. Alieleza kuwa Kanuni ya 10 inatoa utaratibu wa uachishwaji kazi iwapo mfanyakazi yupo katika kipindi cha majaribio. Wakili alisisitiza kuwa mjibu maombi namba mbili hapaswi kunufaika na vifungu vya uachishwaji kazi usio halali. 3 Aliendelea kueleza kuwa hoja ya kuwa mjibu maombi namba mbili alikuwa katika kipindi cha majaribio inajidhuihirisha wazi katika ukurasa wa 2 wa tuzo ambapo DW1 aliambia Tume kuwa mfanyakazi huyo alikuwa katika mud awa majaribio na Ushahidi huo haukupingwa kwa namna yoyote. Alisisitiza kuwa Tume ilipaswa kutambua kuwa hoja yoyote ambayo haijapingwa kwa namna yoyote ile maana yake ni kuwa imekubaliwa hivyo inapaswa kupewa uzito. Kuyapa nguvu maelezo yake Wakili aliirejesha mahakama katika kesi ya Tom Morio vs Athumani Hassan & Others (Civil Appeal 179 of 2019) [2022] TZCA 114 (16 March 2022) na kesi ya Nyerere Nyague vs Republic (Criminal Appeal Case 67 of 2010) [2012] TZCA 103 (21 May 2012). Wakili aliendelea kusesitiza kuwa mjibu maombi namba mbili alikuwa katika kipindi cha majaribio. Alieleza kuwa mfanyakazi aliyepo katika kipindi cha majaribio hawezi kunufaika na vifungu vya kuachishwa kazi isvyo halali kama ilivyoamuriwa katika kesi ya David Nzaligo vs National Microfinance Bank Pic (Civil Appeal 61 of 2016) [2019] TZCA 540 (09 September 2019). Aliongeza kuwa mfanyakazi atakuwa katika kipindi cha majaribio mpaka atakapoambiwa amefaulu ushahidi ndipo atakuwa mwajiriwa rasmi. Kuyapa nguvu maelezo yake wakili 4 alirejea kesi ya Stella Temu Vs. Tanzania Revenue Authority

[2005] TLR 178. Kwa upande wa mshahara Wakili Maricha alieleza kuwa Tume haikuzingatia Ushahidi kwakuwa DW1 alitoa kielelezo DI kinachoonesha kuwa mjibu maombi wa kwanza aliajiriwa kwa mshahara wa shilingi 150,000/= na mpaka anaachishwa kazi mshahara wake ulikuwa shilingi 250,000/=. Alieleza kuwa cha kushangaza Tume ilitumia mshahara wa shilingi 350,000/= ambao haikuwa na uthibitisho wowote. Aliendelea kueleza kuwa Tume ingeongeza umakini kidogo ingebaini Ushahidi wa uongo uliotolewa na PW1. Kwamba alieleza kuwa amefanya kazi kwa mleta maombi kwa muda wa miaka 16 lakini mkataba wake wa ajira (kielelezo DI) kinaonesha kuwa alianza kufanya kazi mwaka 2010 hivyo tukihasabu mpaka pale alipoachishwa kazi, 2020 ni miaka 10 tu na sio 16 kama alivyoambia Tume. Aliongeza kuwa Tume ilishindwa kubaini ukweli kuwa PW1 alikataa kusaini barua za wito kwa makusudi hivyo kwa Ushahidi uliopo aliiomba mahakama itengue maamuzi ya Tume. Mwisho wakili Maricha alieleza kuwa taratibu za kuwaachisha kazi wajibu maombi zilifuatwa kwani walipewa nafasi ya kujitetea kwa maandishi na walikaidi wao wenyewe kama inavyothibitika katika kielezo D3. Aliongeza kuwa waliitwa

katika kikao cha nidhamu lakini pia 5 walikataa kama inavyothibitishwa na kielezo D3 kwa Pamoja. Kwamba kutokana na mazingira hayo yote mwajiri hakuwa na namna nyingine Zaidi ya kuendelea na kikao cha nidhamu bila uwepo wao kama inavyoonekana katika kielelezo D4. Hivyo kutokana na mazingira hayo aliiomba Mahakama itengue maamuzi ya Tume, Akijibu hoja za mleta maombi Bw. Lufasinza aliomba kiapo kinzani kiwe sehemu ya mawasilisho wake. Alieleza kuwa hoja ya kwanza haina nguvu kisheria kwakuwa hapakuwa na sababu za msingi za kuwaachisha kazi waleta maombi. Aliongeza kuwa hoja ya kuwa wajibu maombi walikaidi maagizo ya mwajiri na kukataa kupokea barua ya wito wa kujieleza kutokana na kosa walilofanya haina Ushahidi wowote. Kuhusu hoja ya pili alieleza kuwa imeibuliwa mbele ya mahakama hii na haikuamuriwa Tume. Alieleza kuwa mada yoyote ambayo haikujadiliwa ngazi ya chini ya kimaamuzi haiwezi kuja upya kwenye ngazi ya juu ya maamuzi. Alieleza kuwa hoja hiyo pia haina nguvu. Katika hoja ya mwisho Bw. Lufasinza alieleza kuwa hoja hiyo haina nguvu kisheria kwakuwa utaratibu uliotumika kuwaachisha kazi wajibu maombi haukuwa sahihi. Kwamba mwajiri hakutoa taarifa kwa wajibu maombi kabla ya kufayika kikao cha nidhamu kama ilivyojadiliwa kwa usahihi na mwamuzi katika ukurusa wa 9 na 10 wa Tuzo. Aliongeza 6 kuwa madai ya mleta maombi ya kukataliwa kupokelewa wito wa kikao cha nidhamu hayana msingi kwakuwa kipindi cha kusikiliza kikao cha nidhamu wajibu maombi walikuwa wanashikiliwa na polisi kwa kosa hilo hilo walilokuwa wanatuhumiwa na mleta maombi. Bw. Lufinza alieendelea kueleza kuwa kwa mujibu wa Kifungu cha 35(5) cha Sura ya 366 KM 2019 hata kama wajibu maombi wangepokea na kuhudhuria kikao cha nidhamu bado isingekuwa sawa kisheria kwa mwajiri kuendelea na kikao cha nidhamu wakati wajibu maombi walikuwa wanaendelea na kesi ya jinai kwa kosa hilohilo ambalo walikuwa wanatuhumiwa na mwajiri wao. Alimalizia kwa kueleza kuwa hoja hiyo pia haina nguvu kisheria. Hivyo basi Bw. Lufunzi aliomba maombi haya yatupiliwe mbali kwa ujumla wake. Baada ya kupitia mawasilisho ya pande zote mbili, kumbukumbu za Tume na mahakama Pamoja na sheria mbalimbali mahakama inaona kuwa inatakiwa kutatua hoja zifuatazo; kwanza ni endapi mjibu maombi wa pili alikuwa kipindi cha majaribio, pili endapo mleta maombi alikuwa na sababu za msingi za kuwafukuza kazi wajibu maombi, tatu endapo mleta maombi alifuata taratibu kuwaachisha kazi wajibu maombi na mwisho ni nini stahiki za wadaawa. 7 Nikianza na hoja ya kwanza ya endapo mjibi maombi wa pili alikuwa kipindi cha majaribio, hoja hii imetelewa mkazo na mleta maombi mbele ya mahakama hii. Hata hivyo katika Ushahidi wake DW1 mbele ya Tume alieleza pia kuwa mjibu maombi wapili, Bw. Shabani Tulli alikuwa katika kipindi cha majaribio. Baaada ya kupitia Ushahidi uliotolewa unaonesha kuwa Bw. Shabani Tuli aliajiriwa mnamo tarehe 14/08/2015 kama Mtunza Stoo lakini hakuna mkataba wowote aliopewa. Kisheria ni jukumu la mleta maombi kumpatia mwajiriwa mkataba wa maandishi kama ilivyoielezwa katika kifungu cha 15(1) cha Sura ya 366 KM 2019. Sheria imeendelea kueleza kuwa endapo mwajiri huyo hatampatia mwajiriwa mkataba basi anajukumu la kuthibitisha taarifa za kiajiri za mfanyakazi husika, hii imeelezwa katika kifungu cha 15(6) cha Sura 366 KM 2019. Kama ilivyoielezwa hapo awali katika shauri hili mleta maombi hajatoa mkataba wowote kuthibitisha hoja yake kuwa mjibu maombi wa pili alikuwa katika

kipindi cha majaribio. Hoja hiyo inaonekana kuibuliwa tu mbele ya Tume bi la uthibitisho wowote hivyo haina mashiko. Katika hoja ya pili mahakama inajiuliza endapo mleta maombi alikuwa na sababu za msingi za kuwaachisha kazi wajibu maombi. Katika barua za kusitishiwa ajira (kielelezo D5) mjibu maombi wa kwanza, 8 Mohamed Abdallah Haidary amefukuzwa kwa tuhuma za kuvunja uaminifu kwa kujaribu kutoka na mail ya mwajiri pasina ridhaa ya mwajiri, kukaidi maagizo halali kutoka kwa mwajiri, matumizi mabaya ya nafasi ya ufundi (kumlaghai mtunza stoo ampatie mafuta kinyume cha taratibu za ofisi) na kukaidi kupokea barua ya kutoa maelezo ya tuhuma zilizokuwa zikimkabili. Kwa upande wa Shabani Tuli imeelezwa kuwa amefukuzwa kazi kwa kosa la uzembe kazini kwa kumpatia fundi mafuta oil lita ishirini bila ya kufuata utaratibu wala kupata ruhusa kutoka kwa kiongozi wa kampuni Pamoja na kukaidi kupokea barua ya kutoa maelezo ya tuhuma zilizokuwa zinamkabili. Ni wazi kuwa shauri hili limetokana na tuhuma za wizi wa mafuta uliodaiwa kutokea mnamo tarehe 27/05/2020. Tuhuma hizo zilifikishwa hadi Mahakama ya mwanzo temeke lakini shauri hilo lilifutwa baada ya mleta maombi kutokuhudhuria mahakamani. Nikiangalia Ushahidi uliopo mbele ya mahakama hii naona kuwa unashindwa kuthibitisha tuhuma hizo za wizi uliofanywa na wajibu maombi. Kwamba baada ya kujaribu kufanya wizi huo wajibu maombi walikamatwa na walizi wa getini na kupelekwa kituo cha polisi. Chakushangaza hata mbele ya Tume hakuna mlinzi yeyote alietoa Ushahidi kuthibitisha kutokea kwa wizi huo. Mleta maombi amedai pia 9 kuwa wajibu maombi walikaidi kutoa maelezo ya maandishi juu ya tuhuma hizo. Nikirejea wito wa kutoa maelezo ya kimaandishi (kielelezo D2) hakuna mahali popote kiliposainiwa kupokelewa na wajibu maombi. DW2 alitoa Ushahidi kuwa aliwapelekea wajibu maombi lakini walikataa kusaini. Ni dhahiri kuwa katika taarifa zao za ajira wajibu maombi wanaanuani za makazi yao na hata sanduku la posta hivyo basi, kama kweli walikataa kupokea barua hizo ilikuwa ni wajibu wa mwajiri kutumia njia nyingine zaidi ya kuwapelekea barua hizo ili kupata uthibitisho kuwa kweli wamekataa kupokea. Maandishi pekee katika barua husika kuwa wajibu maombi walikataa kupokea hayatoshi kuwakuta na hatia na kosa la kukaidi maagizo ya mwajiri wao. Hivyo basi, Mahakama inaona hakuna Ushahidi wa kutosha kuthibitisha tuhuma zilizowakabili wajibu maombi kama ambavyo imeamuriwa na Tume. Kuhusu hoja ya tatu ya endapo mleta maombi alifuata taratibu za kuwaachisha kazi wajibu maombi; kama ambavyo imeanishwa hapo juu waleta maombi walifukuzwa kazi kwasababu ya utovu wa nidhamu. Taratibu za kumfukuza kazi mfanyakazi aliekwta na hatia na kosa la utovu wa nidhamu zimeainishwa katika Kanuni ya 13 Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini (Kanuni za utendaji Bora) Tangazo la Serikali Na. 42 la mwaka 2007. Katika shauri hili mleta maombi anadai kuwa aliwataarifu 10 wajibu maombi kuhudhuria katika kikao cha nidhamu hata hivyo walikaidi kufika. Kama ilivyoelezwa hapo awali kuwa hakuna uthibitisho wowote wa kujitosheleza kuwa wajibu maombi walikataa wito na kukaidi maagizo ya kufika katika kikao cha nidhamu. Lakini hata hivyo hata kama wangekubali wito huo na kuhudhuria kikao cha nidhamu mleta maombi alikuwa hana mamlaka ya kuwafukuza kazi wajibu maombi wakati shauri lililopo mbele ya mahakama lilikuwa linaendelea. Vielelezo vinaonesha kikao cha nidhamu kilifanyika tarehe 15/06/2020 (kielelezo D4) lakini shauri

mbele ya mahakama lilifutwa tarehe 03/07/2020. Hivyo basi wakati kikao cha nidhamu kinafanyika wajibu maombi walikuwa bado na kesi ya jinai inaendelea mbele ya mahakama inayohusiana na tuhuma walizokuwa wanaitiwa katika kikao cha nidhamu. Kwa mantiki hiyo kikao cha nidhamu kiliendeshwa kinyume na Kifungu cha 37(5) cha Sura ya 366 KM 2019. Kwa kuzingatia Ushahidi uliotolewa katika shauri hili naunga mkono maamuzi ya Tume kuwa mleta maombi hakuwa na sababu za msingi za kuwafukuza kazi wajibu maombi na wala hakufuata utaratibu katika kusitisha ajira zao. Katika hoja ya mwisho ya nini stahiki za kila upande, mbele ya Tume wajibu maombi waliomba malipo yafuatayo, mshahara wa mwezi ii mmoja badala ya taarifa ya kufukuzwa kazi, mshahara wa mwezi Juni, 2020, mshahara wa siku 13 kwa mwezi July, 2020 wakiwa wanasubiri barua za kufukuzwa kazi, kiinua mgongo pamoja na fidia ya kuachishwa kazi isivyo halali. Katika barua za malipo ya kusitishwa mkataba wa ajira (kielelezo D6) imeelekezwa kuwa wajibu maombi walipwe kiinua mgongo, mshahara wa mwezi mmoja badala ya taarifa ya kufukuzwa kazi, siku walizofanyia kazi pamoja na malipo ya likizo. Hivyo basi kwakuwa madai mengine yamekwisha lipa limebaki dai la fidia ya kuachishwa kazi isivyo halali ambapo nafuu za uachishwaji kazi usio halali zimeanishwa katika kifungu cha 40 cha Sura 366 KM 2019. Katika shauri hili kwakuwa imethibitika kuwa mleta maombi aliwaachisha kazi wajibu maombi isivyo halali naunga mkono maamuzi ya Tume ya kuwalipa wajibu maombi mishahara ya miezi kumi na mbili (12) kama fidia. Nimezingatia mawasilisho ya mleta maombi kuwa Tume ilikosea kufanya hesabu kwa mshahara wa shilingi laki tatu na nusu (TZS 350,000/=) kwa Bw. Mohamed Abdallah. Ni kweli kuwa kwa vielelezo vilivyopo katika jalada husika hakuna Ushahidi wa kuthibitisha malipo hayo ya mshahara. Vielelezo vinathibitisha kuwa mshahara alioanza nao kazi mjibu maombi wa kwanza ulikuwa TZS. 150,000/= na ukapanda 12 hadi kufikia TZS. 250,000/=. Hivyo basi Tume ilijielekeza vibaya kwa kuzingatia mshahara ambao haukuthibitishwa, hivyo mshahara halisi wa kutumika wakati wa kufanya mchanganuo wa malipo utakuwa ni TZS 250,000/- na sio 350,000/- kama ilivyoamriwa na Tume. Kutokana na marekebisho haya, mchanganuo utakuwa kama ifuatavyo:

1. Mohamed Abdallah Haidary $250,000 \times 12 = 3,000,000/-$
2. Shabani Juma Tully..... Tshs. $150,000 \times 12 = 1,800,000/-$ Jumla Kuu ni Tshs. 4,800,000/-
Mwisho kabisa kwakuwa imethibitika kulikuwa na usitishwaji kazi usio halali Mahakama inayathibitisha maamuzi ya Tume baada ya kufanya marekebisho kama ilivyoainishwa hapo juu. Mbali na hilo, maombi haya yanatupiliwa mbali. Imetolewa leo Tarehe 29 Mwezi Agosti, 2022. SiM.MAGHIMBI JAJI 13

Source & reproduction note

Judgment wording, source notices and original paragraph numbers are retained. Esheria supplies the layout and this PDF's page numbers; these are not the source pagination. This is a research copy, not an official or certified court document. Check quotations, citations and publication restrictions against the original source before relying on it.

ORIGINAL SOURCE https://media.tanzlii.org/media/judgment/151111/source_file/kn-solanki-transport-ltd-vs-mohamed-abdallah-haidary-na-mwenzake-2022-tzhcld-881-29-agosti-2022.pdf

CASE PAGE <https://chat.esheria.ai/case-law/tanzania/kn-so-lan-ki-transport-ltd-unfairtermination-tanzlii-2022--6a3ea52b3b1caa912982427d>

Prepared on 14 October 2026 · Esheria